



MAFINGA, MUFINDI NA IRINGA VIJIJINI ZAMPOKEA DKT. SAMIA





RAIS SAMIA KUFUNGUA VITUO VYA KUNUNULIA MAHINDI MAKAMBAKO

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan amesema serikali itafungua vituo vya kununulia mahindi mwezi huu katika wilaya ya Njombe

Akihutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliofurika kumsikiliza leo Makambako, Rais amesema ndani ya mwezi huu serikali itafungua vituo hivyo ili kuwasaidia wakulima kuuza mahindi yao kwa urahisi na bei nzuri ya serikali.

Rais Samia amefafanua kuwa, maeneo ambayo vituo hivyo vitafunguliwa yatatangazwa baadae baada ya serikali kukamilisha maandalizi yake.





SERIKALI KUJENGA TAWI LA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWL. NYERERE MAKAMBAKO

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan, amesema serikali itaanza ujenzi wa Tawi la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kata ya Maguvani, Makambako.

Rais Samia ameyasema hayo leo Makambako wakati akihutubia maelfu ya wakazi wa wilaya hiyo waliokusanyika kumsikiliza.

Rais Samia amesema, fedha za ujenzi huo zipo tayari kutoka benki ya dunia kupitia mradi wa 'Higher Education for Economic Transformation(HEET)'.

Taarifa kutoka katika wilaya ya Makambako zinasema, halmashauri ya mji wa Makambako wilayani Njombe iliingia makubaliano na Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere kujenga chuo hicho Februari mwaka huu.

Ujenzi wa chuo hicho utatekelezwa kwa awamu tatu, ambapo awamu ya kwanza itahusisha uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ya ekari 103, ujenzi wa majengo machache ya msingi kwa ajili ya kuanzisha chuo rasmi na ujenzi wa majengo ya awali yatakayohusisha madarasa, jengo la utawala na ukumbi wa mihadhara ambapo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kuanzia sasa.

Awamu ya pili itahusisha ujenzi wa kituo mahsusi cha mafunzo ya biashara, ujenzi na uanzishwaji wa kituo cha huduma kwa wananchi.

Awamu ya tatu itahusisha upanuzi wa madarasa na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi, upanuzi wa masomo ya shahada za uzamili na uanzishwaji wa kituo cha usimamizi wa mazingira.



RAIS SAMIA KUJENGA KILOMETA TAKRIBANI 100 ZA LAMI NYORORO MUFINDI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan ameaidi kujenga kilometa 94.9 za lami Nyororo wilaya ya Mufindi.

Rais Samia ameyasema hayo leo Septemba 6, 2025 katika wilaya ya Mufindi wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa CCM waliofurika kumsikiliza.

Akifafanua zaidi Rais Samia amesema atajenga kilometa 40.4 kutoka Nyororo hadi Mtwango kwa kiwango cha lami na kazi imeanza mkandarasi yupo eneo la tukio.

Ameongeza kusema kuwa kilometa 54.5 kwa kiwango cha lami zitajengwa kutoka Igowele, Kasanga hadi Jigo.

Rais Samia amewaomba wananchi kuwa watulivu barabara zote hizo zitajengwa na kuisha kwa wakati





DKT. SAMIA KUJENGA VITUO VYA KUUZIA MAHINDI MAKAMBAKO

Mgombea Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, amewaahidi wananchi wa Makambako Mkoani Njombe kuwa kuanzia mwezi Oktoba 2025, Serikali ya CCM itaanza kujenga vituo vya kuuzia mahindi Mkoani humo kama sehemu ya kutoa fursa ya masoko kwa wakulima wa Mkoa huo wa Njombe.

"Mtakapotupa ridhaa ya kurudi madarakani tutajenga vituo vya kuuzia mahindi ikiwa ni namna ya kutoa fursa ya masoko," amesema.

Dkt. Samia ameyasema hayo wakati wa mkutano wake wa Kampeni kwenye soko kuu la Makambako akiwa njiani kuelekea Mkoani Iringa kuendelea na kampeni yake, akiahidi pia kulifanyia kazi ombi la Katibu Mkuu mstaafu wa CCM na Mgombea Ubunge wa Jimbo Mhe. Godfrey Chongolo, aliyeomba mji huo kujengewa bandari Kavu kutokana na umuhimu wake wa kuwa kitovu cha biashara kwa Mikoa ya kusini na nchi za jirani.

"Hili ombi lenu la kuwapatia bandari kavu tutaenda kulifanyia kazi," Mhe. Samia amesema.

Dkt. Samia amebainisha kuwa ameingia Makambako kwa ujasiri mkubwa kutokana na yale yaliyotekelezwa Mkoani Njombe kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita pamoja na mipango ya miaka mitano ijayo, ametumia fursa hiyo kuwaomba kujitokeza kwa wingi Oktoba 29, 2025 ili kuweza kupiga kura na kuchagua viongozi watakaoweza kusogeza mbele maendeleo ya Jimbo hilo la Makambako.



DKT. SAMIA KUNUNUA X- RAY HOSPITALI YA WILAYA YA MUFINDI



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema atanunua X- ray mpya kwa ajili ya kutoa huduma ya mionzi katika hospitali ya wilaya ya Mufindi.

Dkt. Samia ameyasema hayo leo Nyororo- Mufindi wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa CCM kuomba kura kuchaguliwa kwa kipindi kingine.

Rais Samia amesema linapokuja suala la afya, elimu na maji atahakikisha kila mtanzania anapata huduma nzuri na kwa wakati.





DKT. SAMIA: TUTAJENGA STENDI YA KIMATAIFA MAFINGA



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atajenga stendi mpya na ya kimataifa Mafinga.

Rais Samia ameyasema leo Mufindi wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa CCM waliokusanyika kusikiliza ilani ya chama hicho itakayoenda kutelelezwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Amewaomba wananchi wampe ridhaa kuongoza kipindi kingine ili kujenga na kumaliza stendi hiyo kwa kiwango cha kimataifa ili kuhudumia watanzania na mataifa mengine yanayopita katika kanda hiyo.

TUNAZIMA ZOTE TUNAWASHA KIJANI



CCM NI CHAMA KINACHOJALI WANANCHI WAKE





WAFANYAKAZI WA KIWANDA CHA CHAI MUFINDI, KARATASI MGOLOLO KULIPWA STAHIKI ZAO

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema wafanyakazi waliokuwa wamesimamishiwa kulipwa stahiki zao baada ya Mwekezaji wa kiwanda cha Chai Mufindi kuyumba kiuchumi tangu Januari mwaka huu wameanza kulipwa stahiki zao.

Rais Samia ameyasema hayo leo Nyoyoro, Mufindi wakati akihutubia wafuasi wa CCM waliofurika kumsikiliza akiomba kuchaguliwa kipindi kingine.

Rais Samia amesema kuwa, juma lililopita mwekezaji huyo alipata takribani mkopo wa shilingi bilioni nane kutoka katika mabenki na ameanza kulipa stahiki za wafanyakazi ambazo walikuwa wanadai wakati kiwanda kiliposimama kufanya kazi.

Rais Samia ameongeza kuwa, mkopo huo pia utatumika kufufua kiwanda kwa kununua mashine mpya na za kisasa za kuchakata zao hilo.

Katika hatua nyingine Rais Samia ameeleza kuwa, ameunda timu ya kufanya tathmini kwa viwanda na mashamba yaliyosimama kufanya kazi ili ikimaliza kazi yao wenye nayo wanyanganywe na kukabidhiwa vyama vya ushirika nchini.

Ameongeza kusema kuwa iwapo na mwekezaji wa kiwanda cha Chai atashindwa kukiendeleza tena baada ya kupata mkopo atanyanganywa na kukikabidhi chama cha ushirika.

Serikali imejizatiti kulinda zao la chai kwa nguvu zote kwa sababu ni alama ya uchumi wa nchi.

Kwa upande mwingine, Rais Samia amesema, serikali itafanyia kazi madai mapya ya kiwanda cha karatasi cha mgololo ili wahusika walipwe stahiki zao.

Amesema mwekezaji na serikali walishalipa wafanyakazi stahiki zao lakini yameibuka madai mapya hivyo ameunda timu ya kutathimini na yakibainika kuwa kweli wahusika watalipwa stahiki zao.





CCM KUIMARISHA SEKTA YA MADINI GEITA

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Emmanuel Nchimbi, ameahidi kuwa iwapo chama hicho kitapata tena ridhaa ya kuongoza Taifa, Mji wa Katoro maarufu kama Kariakoo ya Geita, itaimarishwa zaidi katika Sekta ya Madini kwa kuongeza mara mbili bajeti ya utafiti ili kufungua maeneo mapya ya uwekezaji.

Dkt. Nchimbi ameyasema hayo leo Septemba 6, 2025, wakati wa kampeni za CCM akibainisha sera na mipango ya chama hicho.

Amesema maendeleo makubwa tayari yamepatikana katika sekta hiyo kwani wakati Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani kulikuwa na leseni 903 za uchimbaji, lakini hadi wiki iliyopita idadi hiyo imeongezeka kufikia 9,774 kwa wachimbaji wadogo.

Ameongeza kuwa kasi ya utoaji leseni itaongezwa ndani ya miaka mitano ijayo ya uongozi wa Dkt. Samia, huku madini adimu yakipewa utaratibu bora wa uchimbaji, na vijana kuhamasishwa kushiriki katika uchimbaji wa madini ya kimkakati.





DKT NCHIMBI: NYAKANAZI KUWA KITOVU CHA BIASHARA MAZIWA MAKUU

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Emmanuel Nchimbi, amesema kuwa chama hicho, endapo kitapata ridhaa ya kuongoza serikali, kitaendelea kuhakikisha mji wa Nyakanazi, wilayani Biharamulo, mkoani Kagera, unakuwa kitovu cha biashara kati ya Tanzania na nchi za Maziwa Makuu.

Dkt. Nchimbi amesema hayo alipokuwa akihutubia mkutano wa kampeni wa CCM katika Kata ya Nyakanazi, akiongeza kuwa serikali imepanga kujenga kituo cha ushuru wa forodha wa pamoja katika mji huo ili kurahisisha shughuli za kibiashara kati ya Tanzania na baadhi ya nchi jirani.

Awali, akiwa katika Kata ya Bwanga, wilayani Chato, mkoani Geita, mgombea mwenza huyo wa urais alisema Serikali ya CCM ijayo itaboresha huduma za jamii; elimu, barabara na afya na hususani kuboresha Kituo cha Afya cha Bwanga.





KISWAGA: ASANTE RAIS SAMIA KWA KUTOA BILIONI 700 KWA WAKULIMA

Mgombea ubunge wa jimbo la Iringa Vijijini kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Ndugu Jackson Kiswaga, amemshukuru Rais Samia mbaye pia ni mgombea Urais kwa chama hicho kwa kutoa ruzuku kwa wakulima wa jimbo la Kalenga mkoani Iringa zenye thamani ya shilingi bilioni 700.

Mgombea ubunge huyo Mhe. Kiswaga, amesema hayo kwenye Mkutano wa Kampeni za mgombea Urais uliofanyika Iringa Vijijini Septemba 6, 2025.

"Mhe. Rais tunakushukuru kwa kuwa umetupatia shilingi bilioni 700 kwa ajili ya ruzuku na kwa kweli umetuheshimisha sana wanakalenga kwa kuwa tumevuna kwa wingi na tuna chakula cha kutosha," Mhe. Kiswaga amesema.

Pia, Mhe. Kiswaga amemshukuru Mhe. Samia kwa kutoa kiasi cha shilingi bilioni 13 kwa ajili ya Kilimo cha umwagiliaji.

Katika sekta ya maji, Mhe. Kiswaga, amesema jimbo la Kalenga lina vyanzo vya maji vingi ingawa ameishukuru Serikali kwa miradi 8 iliyokamilika, nakuongeza kuwa miradi minne iko katika utekelezaji kwa gharama ya shilingi bilioni 8.

Akizungumzia kuhusu sekta nishati, Mhe. Kiswaga amesema tayari vitongoji 340 kati ya 455 vimepata umeme, nakuongeza kuwa bado vitongoji 115 ambapo inaendelea.

Aidha, kwenye miundombinu, Mhe. Kiswaga, amemshukuru Mhe. Samia kwa kuboresha barabara nakutoa mfano wa ujenzi wa barabara ya kuelekea Ruaha National Park uliogharimu bilioni 3.

"Tunakushukuru sana kwa kujenga barabara ya kutoka Iringa Mjini-Kilolo inayopita katika jimbo la Kalenga kwa gharama ya shilingi bilioni 60," amesema.

Mhe. Kiswaga amesema, Serikali ya CCM imejenga barabara kutoka Wenda-Mgama kwa kiasi cha shilingi bilioni 29.

Katika eneo la elimu, Mhe. Kiswaga amesema Serikali ya Mhe. Samia, imejenga shule mpya za sekondari 24 na madarasa 173.





RAIS SAMIA AOMBA MAKUNDI NDANI YA CHAMA KUVUNJWA NA KUWA KITU KIMOJA

Mgombea Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaomba wanachama wa Chama hicho kuvunja makundi yaliyopo kwa sasa ili kuwa na Chama chenye nguvu kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa mwaka huu.

Rais Samia ameyasema hayo leo wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa Chama hicho waliokusanyika kumsikiliza mjini Mafinga.

Rais Samia amesema, “naomba wanaCCM nchi nzima tuvunje makundi tuliyonayo ili tuwe na nguvu na umoja kipindi hiki cha uchaguzi”. Amesema.

Rais Samia amewaasa makada hao kutokuwa kama wafuasi wa vyama vingine ambavyo wameshaparaganyika wakati hata kampeini za uchaguzi hazijaisha.





DANIEL CHONGOLO: BILIONI 43 KUMALIZA TATIZO LA MAJI KATIKA MJI WA MAKAMBAKO

Katibu Mkuu mstaafu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na mgombea ubunge kwa jimbo la Makambako, Daniel Chongolo, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwapatia wananchi wa Makambako suluhisho la upungufu wa maji kwa kuanza ujenzi wa mradi wa maji wenye thamani ya shilingi bilioni 43.

Chongolo, ameyasema hayo katika Mkutano wa Kampeni za mgombea Urais CCM zilizofanyika kwenye mji wa Makambako leo Septemba 6, 2025.

Akimshukuru Rais Samia kwa kutoa kiasi cha shilingi bilioni 43 ili kumaliza changamoto ya maji kwa wakazi wa mji wa Makambako, Chongolo amesema tayari mradi huo umefikia 40%.

“Mji wa Makambako ulikuwa na changamoto ya maji, kwa kutambua hilo umeidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 43 kwa ajili ya kumaliza kabisa changamoto hii kwa wananchi. Hivi sasa mradi huu umefikia 40% na iwapo nitapata ridhaa ya kuchaguliwa kuwa mbunge wa Makambako nitakuwakilisha vizuri ili mradi ukamilike kwa wakati na matokeo yatokee kwa haraka kwa wananchi,” alisema Chongolo





KONA YA ILANI

Kuendelea Kuimarisha
Miundombinu ya Usafiri
na Usafirishaji.





LUKUVI: RAIS SAMIA NI WAKIPEKEE KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mgombea Ubunge katika Jimbo la Isimani mkoani Iringa kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), William Lukuvi amewaambia wakazi wa Iringa kuwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais wa kipekee kwani katika kipindi cha uongozi wake ametekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ambayo haikutimizwa kwa zaidi ya miaka 25.

Lukuvi amesema, yeye ni Mbunge aliyehudumu kwa kipindi kirefu hivyo haoni sababu ya kutokumpongeza Dkt. Samia, kwani amewaleta maendeleo ya kihistoria wananchi.

Lukuvi amesema hayo leo Septemba 6, 2025 wakati wa Mkutano wa kampeni za mgombea Urais kwa tiketi ya CCM, Dkt. Samia unaofanyika Kalenga mkoani Iringa.



#ATATEKELEZA





KEVIN FALLEN



ssh_anatekeleza